

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO
MKUTANO WA TISA
KIKAO CHA TATU

9 NOVEMBA, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TISA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 9 NOVEMBA, 2017

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**30. MHESHIMIWA RUTH HIYOB MOLLEL
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Maboresho ya utendaji wa Serikali za Mitaa yalilenga kuimarisha na kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa kujiendesha kwa kuwapatia Rasilimali watu na fedha za kutosha kutekeleza sera ya ugatuaji wa madaraka:-

Je, Serikali ina lengo gani kuimarisha Serikali za Mitaa ziweze kujiendesha.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

31. MHESHIMIWA MBARAKA KITWANA DAU (MAFIA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara ya kurukia ndege katika Uwanja wa Ndege Mafia kwa awamu ya kwanza kwa ufadhili wa Mfuko wa “Millenium Challenge Account” (MCA):-

Je, ni lini Serikali itajenga jengo la abiria na kuweka taa za kurukia kwenye Uwanja huo.

32. MHESHIMIWA CAPT. ABBAS ALI MWINYI (FUONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ndege za Serikali aina ya Fokker 50 iliyoretwa nchini mwaka 1992 na Fokker 28 iliyoretwa nchini mwaka 1978 ni chakavu na teknolojia zake zimepitwa na wakati. Aidha, Kampuni iliyotengeneza aina hizo za ndege imeshafungwa hivyo upatikanaji wa vipuri vyatuhusu ndege hizo kuwa mgumu sana na gharama kuwa kubwa:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzibadilisha ndege hizo na kuleta mpya;

(b) Je, ni lini Serikali itarekebisha hali ya *hanger* la kuegeshea ndege za Serikali.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

33. MHESHIMIWA RASHID ALI ABDALLAH (TUMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mara nyingi hutumika kwa kutoa mikopo kwa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya jamii:-

Je, ni utaratibu gani wa kisheria unaofanyika ili kuhakikisha fedha za Wanachama zinalindwa.

WIZARA YA KILIMO:

34. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSOKELO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Tunatambua juhudzi za Serikali za kujenga Chuo cha Kilimo na Mifugo katika Kata ya Lufilyo:-

Je, ni lini sasa Serikali itamalizia ujenzi wa Bwalo na nyumba za Walimu ili Chuo hicho kianze kutoa

huduma kwa Wananchi hasa ikizingatiwa kuwa majengo ya madarasa yalishakamilika.

35. MHESHIMIWA JEROME DISMAS BWANAUSI (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Serikali iliahidi kuanzisha mfumo wa “*Commodity Exchange*” ili kuwasaidia wananchi wanaolima Korosho kupata bei nzuri katika misimu husika:-

- (a) Je, Serikali ina kauli gani juu ya kuanza kwa mfumo huo;
- (b) Je, Serikali itatatua vipi suala la kodi nyingi kwa Wakulima wa Korosho inayosabisha kupata bei ndogo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

36. MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (BUKOMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Askari wa Wilaya ya Bukombe wanazo changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa nyumba za Askari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia nyumba Askari hao katika Wilaya ya Bukombe.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

37. MHESHIMIWA DEVOTA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Idadi ya Wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu vya Mkoa wa Morogoro imepungua kutokana na Wanafunzi wengi kukosa mikopo ya Elimu ya Juu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

38. MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Kupitia fursa za Ujenzi wa Mabweni ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwezi Aprili, 2017:-

Je, Serikali imeweka jitihada gani katika kuongeza fursa za ujenzi wa Mabweni kwa Taasisi za Elimu ya Juu hususani Chuo cha Ushirika Moshi Mkoani Kilimanjaro ambapo zaidi ya 70% ya Wanafunzi wanaishi nje ya Chuo.

IV. KAULI ZA MAWAZIRI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

VI. KAMATI YA MIPANGO:

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
9 NOVEMBA, 2017**

**S.N. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**